

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao Cha Tano - Tarehe 30 Januari, 2010

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009

(The National Security Council Bill, 2009)

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema, leo Siku ya Jumamosi hatutaanza na kipindi cha maswali kwa sababu tumetengua Kanuni ili tuweze kukamilisha kazi nyingine ambazo zimezidi; kwa hiyo, tunakwenda moja kwa moja kwenye Muswada.

Sasa namwita mtoa hoja awasilishe Muswada. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora).

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 (*The National Security Council Bill, 2009*), sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuungana na wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Mheshimiwa Vita Kawawa na Familia ya Marehemu Mheshimiwa Mzee Rashid Mfaume Kawawa, kwa kuondokewa na baba yao, Mzee wetu Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa. Pole hizo pia nazitoa kwa Watanzania wote kwa sababu Marehemu Mzee Kawawa ni mmoja wa Viongozi Waasisi la Taifa letu. Aidha, napenda pia kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na wananchi wote wa Jimbo la Ruangwa kwa kuondokewa na mpendwa wao na Mbunge wao, Marehemu Sigfrid Ng'itu. Naomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za Marehemu pahala pema peponi na awajalie ndugu wa Marehemu moyo wa subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama hapa na kuwasilisha Muswada huu muhimu kla Taifa letu.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuuchambua Muswada huu na kutoa maoni yake ambayo yamesaidia sana katika kuuboresha. Napenda kuwashakikishia kwamba, maoni na michango yenu vimezingatiwa. Pia napenda kuwashukuru kwa dhati wadau mbalimbali kwa michango yao ambayo pia imezingatiwa. (*Makofi*)

Aidha, naishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushauri wao katika kuuandaa Muswada huu na hatimaye kufikia hatua ya kusomwa mara ya pili. Shukrani pia ziende kwa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kutunga Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa, lenye sura ya Jamhuri ya Muungano na litakuwa na muundo wenye ngazi ya Taifa na Kamati ya Usalama katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi na majukumu ya Baraza la Usalama la Taifa na Kamati za Usalama ni kuandaa mikakati na mbinu za kudumisha ulinzi na usalama nchini na katika maeneo husika. Kamati pia zitabaini, kuainisha na kuchambua matatizo ya kijamii na kiutendaji, yanayotokea katika Mkoa na Wilaya na yanaweza kuhatarisha usalama na kushauri Mamlaka husika hatua za kuchukua. Inapendekezwa pia kuweko utaratibu wa uratibu wa taarifa za siri utakaowezesha watu binafsi, taasisi za umma na taasisi binafsi, kushiriki kuchunguza mienendo ya wakazi wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu na kuziwasilisha kwenye Mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tano zifuatazo:-

Sehemu ya kwanza, inapendekeza masharti ya awali kama vile jina la sheria inayopendekezwa, matumizi ya sheria na tafsiri ya maneno na misamiati itakayotumika.

Sehemu ya pili, inaanizisha Baraza la Usalama la Taifa na inapendekeza kazi na majukumu ya Baraza. Vilevile inapendekeza kuwepo kwa Sekretarieti ya Baraza na kuainisha kazi za Sekretarieti.

Sehemu ya tatu, inaanizisha Kamati za Mikoa na Wilaya na inapendekeza Wajumbe wa Kamati hizo. Kazi za kila ngazi pia zimeainishwa katika sehemu hii.

Sehemu ya nne, inaweka adhabu kwa Mjumbe atakayekiuka matumizi ya taarifa za kiusalama ambazo atazijua kutokana na nafasi yake kama Mjumbe. Kadhalika, sehemu hii inaweka utaratibu wa Vikao vya Kamati za Usalama wa Taifa kama nyongeza ya utaratibu ulioainishwa katika jedwali. Wajibu wa kila Kamati ya Usalama kutoa Taarifa juu ya shughuli zake, umeelekezwa pamoja na masharti kuhusu gharama za uendeshaji wa Baraza la Usalama la Taifa na Kamati zake. Aidha, Waziri mwenye

dhamana ya masuala ya usalama la Taifa, amepewa mamlaka ya kutengeneza Kanuni za Kiutendaji na mambo yatokanayo na masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano, inapendekeza kufanya marekebisho madogo katika sheria tofauti tano kwa lengo la kuyaainisha masharti ya sheria hizo na masharti ya Sheria ya Baraza la Taifa inayopendekezwa. Sheria hizo ni *The National Security Council Act, 2009 ; Tanzania Inteligence and Security Service Act, Cap. 206 ; The National Defence Act, Cap. 192 ; The National Service Act, Cap. 193* na *The Disaster Relief Co-ordination Act, Cap. 242*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, baada ya kukamilisha kazi ya kuuchambua Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 (*The National Security Council Bill, 2009*), kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), tarehe 15 Oktoba, 2009, Kamati ilikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), pamoja na Wataalam wa Serikali. Katika Kikao hicho, Kamati ilielezwa kuwa Muswada huu kwa ujumla wake unapendekeza kutunga Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa lenye sura ya Jamhuri ya Muungano, ambalo litakuwa chini ya Uenyekiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa, Baraza la Usalama la Taifa (*BUT*), liliundwa rasmi tarehe 15 Mei, 1992 kuchukua nafasi ya iliyokuwa Tume ya Ulinzi na Usalama ya Chama cha Mapinduzi. Lilipoundwa Baraza hili, liliwekwa chini ya Uenyekiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Katibu wake. Chombo hiki kimekuwa kikitumika kama kiunganishi baina ya Wanasiwa na Wataalam katika masuala yote yanayogusa ulinzi na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ufanuzi uliotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), Kamati ilielezwa kuhusu Muundo wa Baraza kuwa na ngazi ya Taifa na Baraza la Usalama la Zanzibar ambalo litakuwa chini ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika Muswada ulioletwa awali, Serikali ilipendekeza kuwa Baraza la Usalama la Zanzibar litakuwa linatoa taarifa za shughuli kwa Baraza la Usalama la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, Kamati ilielezwa kuhusu sehemu kuu tano za Muswada zilizohusu masharti ya awali, kuanzishwa kwa Baraza la Usalama la Taifa na mapendekezo kuhusu kazi na majukumu ya Baraza, Wajumbe wa Kamati za Usalama ngazi ya Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Kijiji, pamoja na majukumu ya kila ngazi. Hata hivyo, katika Muswada tunaoujadili leo, Kamati za Usalama zinaishia ngazi ya Wilaya na Mkoa. Sehemu nyingine ya Muswada huu inapendekeza utaratibu wa Vikao vya Kamati za Usalama na sehemu ya mwisho inapendekeza marekebisho katika Sheria tano ambazo ni Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa, Sura ya 406 (*The Tanzania Intelligence and Security Service Act, Cap. 406*); Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sura ya 192 (*The National Defence Act, Cap. 192*); Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, Sura ya 193 (*The National Service Act, Cap. 193*); Sheria ya Uraia wa Tanzania, Sura ya 357 (*The Tanzania Citizenship Act, Cap. 357*); na Sheria ya Utaratibu wa Maafa, Sura ya 242 (*The Disaster Relief Co-ordination Act, Cap. 242*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya Kamati kuzama kwenye kuuchambua Muswada huu Ibara kwa Ibara, tulipata nafasi ya kusikiliza maoni ya Wadau. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, wadau mbalimbali walialikwa kutoa maoni yao mbele ya Kamati. Ofisi ya Bunge ilitoa matangazo kwa umma na kutaja tarehe ya kusikiliza maoni ya wadau kuhusu Muswada huu. Tunawashukuru *National Organization for Legal Assistance (NOLA)* na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Right Centre*), kwa mchango mkubwa kwa Kamati wakati tulipokutana na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 Novemba, 2009 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, ilifanya kikao cha pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili kuendelea kuufanyia marekebisho Muswada huu. Katika kikao hicho kilichofanyika Mjini Dodoma, Mheshimiwa Waziri alitoa ufanuzi kuhusu maeneo yaliyopendekezwa kwenye kikao cha tarehe 15 Oktoba, 2009 kilichofanyika Mjini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kuzingatia maoni ya msingi ya wadau na yale ya Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Serikali iliomba muda ili kuufanyia kazi zaidi Muswada huu muhimu kwa usalama wa Taifa letu. Katika hatua hii, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kuujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 13 Januari, 2010 Kamati ilikutana tena na kuujadili Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009, baada ya kutangazwa upya kwenye Gazeti la Serikali, Toleo la tarehe 11 Desemba, 2009 na kuleta kwa mara nyine kwenye Kamati. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati iliupitia na kuuchambua kwa kina Ibara kwa Ibara na kukubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa ujumla, pamoja na kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchambua Muswada huu pamoja na hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe na kujibiwa na upande wa Serikali, Kamati ina

maoni na ushauri katika kuuboresha zaidi Muswada huu. Baada ya maeleo niliyoyatoa, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mapendekezo ya Serikali kuhusu Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa ni mazuri na Sheria hii itasaidia sana kurasi misha mambo mengi muhimu kuhusu uandaaji wa mikakati na mbinu za kudumisha Ulinzi na Usalama, uainishaji na uchambuzi wa matatizo ya kijamii na kiutendaji, pamoja na kuweka utaratibu rasmi wa gharama za kuendesha Baraza la Usalama la Taifa na Kamati zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria inayopendekezwa itatumwiwa pia na watu wengine ambao kitaaluma hawana maarifa kuhusu Sekta ya Ulinzi na Usalama, Kamati inashauri kuwa, Ibara ya (3) itaje tafsiri ya maneno *Operational level* ili kuepuka utata unaopatikana katika Ibara ya 2(2) yenye maneno *this Act shall not apply to Security matters at operational level*. Aidha, kwa kuzingatia kuwa Magereza ni miiongoni mwa vyombo vinavyotekeleza majukumu ya kiulinzi na usalama, Kamati inashauri kuwa tafsiri ya maneno *Defence and Security Organs* ijumu ishe Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchambua Ibara ya (3) ya Muswada huu, Kamati pia ilibaini kuwa neno “*Security*” limetajwa kuwa na maana kama ilivyofasiliwa katika Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura ya 407. Hata hivyo, ukweli ni kuwa neno “*Security*” limefasiliwa katika Ibara ya (3) ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa Tanzania (*The Tanzania Intelligence and Security Service, Act Cap. 406*). Ili kutoa maana ya neno “*Security*” kama ilivyokusudiwa, Kamati inashauri kuwa, Ibara ya (3) ya Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa itafsiri neno “*Security*” kwa kuweka maneno “*has the meaning ascribed to it under the Tanzania Intelligence and Security Service Act*” badala ya maneno “*has the meaning ascribed to it under the National Security Act*.”

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6(1), inataja Sekretarieti ya Baraza la Usalama la Taifa ambapo Magereza haitajwi katika Sekretarieti hiyo. Ni maoni ya Kamati kwamba, kwa kuwa Magereza ni miiongoni mwa vyombo muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Usalama la Taifa, ni vyema Ibara ya 6(1) ikajumuisha Magereza katika Sekretarieti ya Baraza la Usalama la Taifa. Aidha, Ibara ya 7(2) imeiruhusu Sekretarieti ya Baraza la Usalama la Taifa kumualika mtu ye yote kwa ajili ya kupata ushauri katika jambo linalojadiliwa. Kuhusu ibara hii, Kamati inashauri kuwa Sheria iweke namna ya kuwazuia wataalamu walioalikwa kwenye vikao vya Sekretarieti hiyo kutoa habari kuhusu mwenendo, uamuzi na makubaliano yaliyofikiwa ndani ya Sekretarieti. Ushauri huu vile vile unahusu Ibara ya 8(3) inayohusu Kamati ya Usalama ya Mkoa na Ibara ya 10(3) inayohusu Kamati ya Usalama ya Wilaya kualika mtu ye yote kwa ajili ya ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipopitia Ibara ya 8(1) inayotaja kuwepo kwa Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya, ilibaini kuwa Maafisa wa Magereza wa Mikoa na Wilaya hawakutajwa kuwa Wajumbe katika Kamati za Usalama. Kwa kuwa Majukumu ya wataalam hawa yananasibiana kwa karibu zaidi na majukumu ya Kamati

za Usalama zinazoanzishwa chini ya Ibara hii, Kamati inashauri kuwa maafisa hawa watajwe kuwa Wajumbe wa Kamati za Usalama katika ngazi walizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Kamati inalitolea ushauri ni kuhusu kazi za Kamati za usalama za Mkoa na Wilaya zinazotajwa katika Ibara ya 9 na Ibara ya 11 za Muswada huu. Kamati inashauri kuwa, masuala ya biashara haramu ya binadamu, ujisadi, haki za makundi maalumu kama vile walemovu, wanawake na watoto na haki za binadamu, yatajwe katika orodha ya kazi za Kamati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya Muswada huu inahusu utaratibu wa Vikao vya Kamati za Usalama. Pamoja na mambo mengine, moja ya mambo yanayopendekezwa katika sehemu hii ni utungaji wa Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa. Ibara ya 16 inampa Waziri uwezo wa kuandaa Kanuni za kiutendaji na mambo yatokanayo na masharti ya Sheria inayopendekezwa. Tafsiri ya “Waziri” katika Ibara ya (3) inatolewa kwa kifungu cha maneno: “*‘Minister’ means the Minister responsible for the National Security.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki cha maneno kinaonesha kuwa Waziri katika Sheria hii ni Waziri mwenye dhamana ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa vyombo vya Usalama unahuishisha Wizara kadhaa kama vile Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Ofisi ya Rais (Utawala Bora). Kamati inashauri kuwa ili kuwa bayana zaidi kuhusu Waziri anayepewa mamlaka ya kutengeneza Kanuni hizo, Sheria imtaje Waziri mwenye dhamana ya Idara ya Usalama wa Taifa Tanzania (*Tanzania Intelligence Service*), badala ya kutaja Waziri mwenye dhamana ya Usalama wa Taifa, dhana ambayo ni pana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo, Kamati pia ilizingatia umuhimu wa lugha na matumizi ya Sarufi kwa ujumla. Katika Ibara ya 18(b) ya Muswada, Serikali inapendekeza marekebisho ya Ibara ya (5) ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa Tanzania (*Tanzania Intelligence and Security Service Act*). Katika mapendekezo hayo, kifungu cha maneno “*The Council*” kinawekwa kati ya maneno “*the*” na “*Minister*” na kufanya Kifungu kipywa kusomeka “*The Council Minister*” ambacho hakitoi maana inayoeleweka. Kamati inashauri kuwa, katika Ibara ya 18(b)(1) ya Muswada huu, neno “*the*” baada ya neno “*phrase*” liondolewe na neno “*and*” lionezwe baada ya neno “*Council*” na kufanya kifungu kipywa kisomeke “*The Council and The Minister.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, hayo ndiyo maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada huu. Aidha, kwa kuwa majukumu ya Baraza la Usalama la Taifa yanategemea sana kanuni za kiutendaji chini ya Sheria itakayotungwa, Kamati ina maoni kuwa umakini mkubwa unahitajika katika utungaji wa Kanuni hizo. Aidha, Elimu ya kutosha itolewe kwa wahusika ili kufikia madhumuni yaliyokusudiwa wakati wa kuandaa Muswada wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Aidha,

nimshukuru Mheshimiwa Sofia M. Simba, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora) na Wataalamu wa Serikali, kwa ushirikiano na ufanuzi walioutoa kwa Kamati yangu mara zote Kamati ilipokutana na kufanikisha kukamilika kwa kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa michango yao ya kina iliyowezesha kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhan Athumani Maneno - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Rajabu H. Juma, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma Maghimbiri, Mheshimiwa Yusuf R. Makamba, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Salim Y. Mohamed, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda pia kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu wa Kamati hii; Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Elihaika Mtui, chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 (*The National Security Council Act, 2009*). Kabla ya yote, naomba kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nguvu na ari ya kuweza kusimama hapa nikiwa mzima na kutoa maoni haya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 53(6)(c), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuingia kwenye Muswada, naomba uniruhusu nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Watanzania wote na hasa wapiga kura wangu wa Jimbo la Micheweni, ambao wamebahatika kuuona mwaka huu wa 2010 wakiwa na afya njema. Pia naomba kutoa salamu za pole kwa Watanzania wote ambao wamepatwa na majonzi ya kuondokewa na wapenzi wao au kupatwa na majanga mbalimbali katika kipindi cha kumaliza mwaka 2009. Mwenyezi Mungu, awape moyo wa subira na uvumilivu, hiyo yote ni mitihani tunayopewa sisi wanadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa sana, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, natoa pongezi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kukubali kwa kauli moja kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari (Kiongozi wa Upinzani Barazani), hoja ambayo chimbuko lake ni Maridhiano kati ya Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Amani Karume, pamoja na Mheshimiwa Maalim

Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (*CUF*) ili kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ambayo itajenga mustakabali mzuri wa kiulinzi na usalama na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Tanzania tuna sheria mbili zainazohusu usalama; moja ni Sheria ya Usalama wa Taifa ya Mwaka 1970 (*National Security Act, 1970*), naomba kunukuu maudhui ya Sheria hiyo: “*An Act to make better provision relating to state security; to deal with espionage, sabotage and other activities prejudicial to the interests of the United Republic; and for purposes incidental thereto or connected therewith*”. Sheria ya pili ni ile ilioanzisha Idara ya Usalama wa Taifa ya Mwaka 1996 (*Tanzania Intelligence and Security Service Act, 1996*), naomba ninukuu maudhui yake: “*An Act to establish the Tanzania Intelligence and Security Service and make provision for other matters relating to it.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi sheria zote bado zipo, japokuwa kuna upungufu wa hapa na pale kutokana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii, yaliyotokea nchini na au yanayoendelea kutokea katika ulimwengu mzima na kuzifanya sheria hizo kutokukidhi matakwa ya sasa. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa ni tatizo gani hasa lililojitekeza au upungufu uliojitekeza hadi kupelekea kuletwa kwa Muswada huu wa Sheria wakati huu? Kwa kuangalia maudhui ya Sheria mbili za Usalama nilizozitaja hapo juu na kwa kuangalia kifungu cha pili cha Muswada huu ni dhahiri kuwa, kuna umuhimu mkubwa kuwa na Sheria moja tu ambayo itaunganisha Sheria zote ili kuondokana na uundwaji wa taasisi nyingi ambazo zitakuwa zinakinzana katika utendaji wa kazi zao. Jambo la msingi ni kutunga kanuni ambazo zitaweka wazi matakwa yote ya usalama wa nchi. Kambi ya Upinzani haioni haja ya kuwa na Sheria tatu tofauti ambazo hatimaye italeta mkanganyiko wa kiutekelezaji bila sababu yoyote na au kuwa na Sheria nyingi zenye kushughulikia jambo lile lile na hivyo kupunguza ufanisi unaotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo kuu la sheria hizo ni kulinda maslahi ya nchi yetu, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka Sheria moja tu ya Usalama wa Taifa na iwekwe wazi Idara itakayokuwa inalinda usalama wa nchi yetu. Si sahihi kuwa na mlolongo wa vyombo vyta usalama kwa usalama wa nchi, kwani kuna wakati tutaifikisha nchi katika hali mbaya kwa kukosa chombo sahihi kinachotoa ushauri wa mwisho kuhusu usalama wa nchi na mambo ya usalama yanahitaji maamuzi kufanyika kwa kasi kubwa. Vyombo vyta usalama ni muhimu sana katika ulimwengu wa sasa hasa katika kutazama kwa makini masuala yote ya uwekezaji unaokuja kuwekezwa Tanzania, yaani wawekezaji kufanyiwa *background work before investing in our country*. Pia ni kazi ya vyombo vyta usalama wa Taifa kujua ni mahitaji gani (mazao yetu ya kilimo, misitu na madini), ambayo Tanzania inaweza kuuza nje kwa bei nzuri. Hili ni muhimu sana kutokana na ushindani uliopo sasa unaotokana na ushirikiano wa Kikanda unaopigwa chapuo na mataifa makubwa Duniani (*Not only the strong will survive but only the braves*), kwa mantiki hii ni bora tujipange kabisa siyo kesho tuanze kutoa visingizio visivyo na msingi wowote.

Aidha, usalama wa Taifa, pia unaangalia utendaji au mwenendo mzima wa uendeshaji wa nchi kwa maslahi ya Taifa. Kimsingi, Kambi ya Upinzani inashangaa,

wakati tunao mtandao mpana sana wa usalama wa Taifa, ni kwa nini matukio ya kifisadi ndani ya *BoT* au kwenye *Deep Green Finance Co. Ltd, Mwananchi Gold Company* na *TANGOLD* yameweza kufanyika, wakati mtandao wa usalama wa Taifa upo na kila mwaka unatengewa mabilioni ya fedha ndani ya Bunge lako Tukufu!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa msingi huu, Kambi ya Upinzani inatoa tahadhari kubwa sana, tunapotunga sheria hii ni muhimu kuangalia tulishindwa wapi na kupaimarisha badala ya kuwa na sheria inayoanzisha Chombo kingine. Kuanzishwa kwa chombo peke yake hakutasaidia usalama wa Taifa, iwapo Sheria zilizopo zinatoa nafasi kwa uhalifu unaohatarisha usalama wa Taifa kutendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama idara hizo zipo kweli ni kwa vipi tunashindwa kuzitumia kwa manufaa yetu; tunapata wawekezaji matapeli, tunashindwa kujua mwelekeo wa bei katika masoko ya nje? Ufisadi mkubwa sana unatendeka ndani ya nchi kupidia vyombo muhimu na vikubwa kama Benki Kuu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imefurahi sana kama ilivyokuwa ikisema kila mara kuwa, Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya haziko kisheria. Kwa kuleta sheria hii, tumethibitisha sasa kuwa hilo lilikuwa kweli na Wakuu wa Mikoa na Wilaya wamekuwa wakifanya maamuzi makubwa kupidia Kamati zao za Ulinzi na Usalama, vyombo ambavyo havikuweko kisheria. Kambi ya Upinzani, inadhani ingelikuwa busara kupima na kufanya Tathmini ya kina ya matumizi ya Kamati hizo kabla ya kutunga sheria mpya inayoanzisha Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya. Ni hatari sana kuanzisha vyombo ambavyo havijafanyiwa utafiti wa kina. Kama umefanyika, basi ni vizuri taarifa na tathmini hiyo iwekwe hadharani. Katika mfumo wa Vyama Vingi ni hatari sana kuanzisha vyombo hivyo, kwani hata kabla havijaundwa rasmi vimekuwa vikutumika vibaya; je, baada ya kuvihalalisha kisheria bila kinga sahihi ndani ya sheria hiyo ya matumizi mabaya hali itakuwaje? (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kudumisha amani na utulivu katika nchi hii kama ambavyo alituachia Muasisi wa Nchi yetu, Mwalimu Nyerere. Mabaraza haya yanayooundwa ni bora yaishie angalau katika ngazi ya Mikoa kwa lengo la uratibu tu, ingawa tunashukuru kuwa yamepunguzwa kutoka vijiji hadi kufikishwa ngazi ya wilaya na mkoa.

Kamati hizi kushuka chini ilikuwa ni kukiuka Ibara ya 146(2)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ninanukuu: “Bila kuathiri maelezo ya jumla yaliyomo katika Ibara ndogo ya (1) ya Ibara hii, kila chombo cha Serikali za Mitaa, kwa kuzingatia masharti ya Sheria iliyokianzisha, kitahusika na shughuli zifuatazo: 146(2)(b) “Kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi”. Kuundwa kwa Kamati ngazi ya Wilaya pia ni kunyume kabisa na dhana nzima ya kupeleka madaraka kwa wananchi (*D by D*), kwani kwa muundo wa sasa Kamati hizi zinakuwa chini ya mfumo wa Serikali Kuu na siyo mfumo wa Serikali za Mitaa, yaani Halmashauri.

Muundo huu wa Serikali Kuu kuendelea kumomonyoa madaraka ya Serikali za Mitaa, haukuliki wakati huu ambapo Serikali Kuu inahubiri sana dhana ya Kuepeleka

Madaraka kwa Wananchi; jambo ambalo linaendana sana na Katiba Ibara ya 8. Kambi ya Upinzani inaona muundo huu wa Kamati za Ulinzi na Usalama kushuka chini zaidi ya Mkoa ni kuitumbukiza nchi katika balaa kubwa ambalo tutakuja kujilaumu na kujuta hapo baadae, kwani matumizi mabaya ya Kamati za Ulinzi na Usalama yamekwisha kuonekana katika maeneo kadhaa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 4(2) cha Muswada kinahusu Wajumbe wa Baraza la Usalama la Taifa. Kambi ya Upinzani baada ya kukiangalia na kufanya utafiti katika nchi nyingine, imegundua kuwa Tanzania hatuwezi kuwa peke yetu, kwani ni muhimu kuangalia wenzetu wamefanyeje; faida na madhara ya mfumo wao ni nini; na pia si vema kufanya majaribio mambo mapya ambayo hayajafanyiwa utafiti wa kina kwani tutakuwa tunachezea maisha ya Watanzania. Sisi ndio tunaanzisha Baraza hili leo, lakini wapo wenzetu wamekuwa na mfumo huu kwa miaka mingi na hivyo mifumo hiyo imekuwa *tested*.

Baraza hili ni la kulinda maslahi ya Taifa na halitakiwi kubagua viongozi kwa misingi yoyote ile. Hivyo, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, kama wenzetu wa Pakistani ambavyo Spika wa Bunge lao na Kiongozi wa Upinzani katika Bunge ni Wajumbe katika Baraza hilo; Kambi inashauri Viongozi hao wawe ni Wajumbe pia katika Baraza hili linaloundwa kutokana na nafasi zao katika jamii ya Tanzania na katika kuimarisha ushirikiano mzuri baina ya utendaji wa mihimili mikuu ya dola. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada Kifungu cha 5(2)(a) na (d) yametumika maneno *National interests* (maslahi ya Taifa). Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tafsiri ya maneno hayo, kwani sasa matakwa ya wale walio madarakani ndiyo yanayotafsiriwa kama ni *National interests* badala ya ustawi wa jamii katika tafsiri pana, kwani jamii imegawanyika katika makundi mbalimbali ambayo wananchi wanaona kuwa ni maslahi ya Taifa kwa mtazamo wao. Kuacha kuweka Tafsiri ya neno hilo kwa Chama kinachotawala kwa wakati huo ni kuhatarisha usalama wa Taifa, ambao ndio lengo kuu la Sheria hii. Neno *National Interests* ni neno pana na inafaa kabisa kuwekewa mipaka ili lisiweze kutumika vibaya, kwani wakati Nelson Mandela anawekwa gerezani, ilikuwa pia maslahi ya Taifa. Tanzania tusitumbukie kwenye mtego huo huo.

Aidha, katika Kifungu cha 5(2)(g) yametumika maneno *enemies of the state* na katika Muswada wote haikutolewa tafsiri ya maneno hayo ni nini. Adui wa Taifa ni yule anayetishia mamlaka ya Rais; na je, wale ambao wana mtazamo tofauti (*ideologically*) na chama kilicho madarakani nao wanawekwa katika kundi hilo? Kama ndiyo hivyo; huku si ni kuhalalisha kuuawa kwa demokrasia ya mtu kuwa na uhuru wa kushiriki katika chama anachoona kinamfaa (kuwa na Vyama Vingi vya Siasa)? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa umakini vifungu hivyo, unajiuliza je Baraza linachukua kazi za Polisi, Kikosi cha Uokozi, Zima Moto na JWTZ? Vinginevyo, hii ni aina nyingine ya kulifanya Bunge kuhalalisha matumizi yasiyo na tija ya fedha za walalahoi kwa kutapanya rasilimali chache zilizopo. Jambo la pili kwa hilo ni kuwa, kuna kitengo maalum chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kinachoshughulikia usalama wa Serikali na pia Kitengo cha Maafa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 6(1) kinachohusu Wajumbe wa *Secretariat* kimemtaja mtu kuwa *coordinator*, lakini katika Muswada mzima huyo *coordinator* na wasaidizi hawakutolewa maelezo ni sifa gani wanakuwa nazo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka wazi sifa za huyo *coordinator* na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15 cha Muswada kinahusiana na gharama za Baraza. Kwa muundo wa Baraza ulivyo, gharama zote za kamati zinatakiwa zilipwe kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali (*Consolidated Fund*); ni dhahiri kuwa hii itaongeza matumizi ya Serikali na kuzidisha mzigo kwa wananchi badala ya kuwasaidia. Matumizi haya ya fedha hayatakuwa na tija kwa mwananchi na udhibiti wa matumizi yake pia utakuwa mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na umuhimu wa kazi za Baraza hili, Kambi ya Upinzani inapendekeza muundo wa Baraza uwe kama ifuatavyo kwa manufaa ya Taifa:-

Kwanza, liwe ndilo chombo cha juu, chini yake kuwe na:-

(i) Kamati itakayoundwa na Watendaji Wakuu katika Serikali (*Strategic Policy Committee*) ambayo itakuwa kazi yake ni kuangalia masuala ya sera za nchi kuhisiana na mwelekeo wa dunia ulivyo kwa kipindi hicho na kwa baadae.

(ii) Kuwepo na Kamati ya Wataalam wa masuala ya usalama (*Joint Intelligence Committee*) ambayo katika Muswada inaitwa *Secretariat* na itahusisha Wataalam wa Ulinzi na Usalama (Wakuu wa vyombo hivyo).

(iii) Mwisho, Kamati au Bodi ya Usalama ya Taifa ya Ushauri (*National Security Advisory Board*), hii itahusisha wajumbe ambao wako nje ya Serikali lakini wana utaalami au ni wajevi wakuu katika fani za usalama wa nje na ndani, sera za nje, uchumi na biashara, fedha na teknolojia kwa upana wake. Hivyo basi, Bodi itakuwa na jukumu la kutoa mwelekeo wa nchi kiulinzi na kiuchumi kwa miaka miwili au mitatu mbele na kutoa tahadhari nini kinatakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wenye viti wa Kamati hizi tatu kama tulivyoshauri ndio watakaokuwa wanaingia kwenye Baraza hili la Ushauri, ambalo litakuwa linafanya vikao vyake chini ya Uenyekiti wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha na nawashukuru wote kwa kunisikiliza. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ninakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji wanenye na kama mnavyojua leo ni nusu siku, kwanza nitamwita Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Anthony Diallo, atafuatiwa Mheshimiwa Ponsiano Nyami, halafu atamalizia Mheshimiwa Shellukindo kama hawapo wengine.

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niwe mchangiaji wa kwanza katika hoja iliyoko mbele yetu, inayohusu Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nieleze kutoridhishwa kwangu na Muswada huu kwa sababu unavunja mantiki yote ya Baraza la Ulinzi na Usalama. Baraza la Ulinzi na Usalama ni chombo cha juu zaidi katika nchi ambacho chini ya usimamizi na maelekezo ya Rais, kinaweza kikavunja agizo lolote la chombo kingine chochote. (*Makofi*)

Sasa ukiangalia katika sehemu ya pili *there is established a Council to be known as the National Security Council* na *the Council shall consist of the following members;* una watu pale Mawaziri zaidi ya kumi. Tunachojaribu kufanya hapa ni kuunda *cabinet* ya pili na Baraza la Ulinzi la Usalama la Taifa haiwezekani ikawa *cabinet* ya pili. (*Makofi*)

Kwa mawazo yangu nilidhani kwamba, Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa lingekuwa na hawa wafuatao; kwanza ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi basi. (*Makofi*)

Hawa Waheshimiwa wengine wote wataitwa kulingana na suala ambalo linajadiliwa pale, hiyo ndiyo tutakuwa tumesema kwamba, chombo hiki kweli ni cha Kitaifa kwa sababu wanaokaa pale ni wale Viongozi wa Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mimi *ni-register* upinzani wangu kwamba, Baraza hili ni kubwa na tukiendelea nalo hili litaacha kuwa Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa bali ni suala la kisiasa na kila litakalokuwa linajadiliwa pale tutalikuta kwenye magazeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni *point* yangu ya kwanza. Halafu kwenye ukurasa wa tano, *sub-para (6)*; “*The decision of the Council shall be by vote of majority. The Council may make rules of procedure on the conduct of its business.* Hapa tunachofanya ni kutia maji madaraka ya Rais; Rais ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa nchi hii. Sasa mnamuundiaje chombo ambacho baadaye kitasema Mheshimiwa Rais pamoja na ukamanda wako *in chief* mimi napingana haiwezekani; tumekubali Rais awe Rais kwa hiyo ana *Executive Powers* zake, pamoja na hizo ni kuwa *commander in chief*. Kwa hiyo, hilo ni mojawapo ya *point* ambazo nazipinga; kwa nini Baraza hili lisiwe kubwa namna hii? (*Makofi*)

Kifungu cha 5(b) kilichopo ukurasa wa sita *kinazungumzia review policies of defense security foreign affairs and other* hii bado itakuwa ni kwenda kinyume cha *mandate* aliyopewa Rais ya kuunda Baraza la Mawaziri na kumpa Waziri anayewajibika madaraka ya kuendesha Wizara hiyo. Sasa mnapomuundia tena chombo kinachomshauri Rais, hii itakuwa inakwenda kinyume na suala zima la *Good Governance*. Kwa ujumla,

ninachokiona hapa, Muswada huu umetengenezwa ili kuipa idara fulani kipaumbele ili uonekane katika masuala ya ulinzi na usalama; hii ni hatari. (*Makofi*)

Mimi ninachoelewa ni kwamba, unapokuwa na Baraza la Ulinzi na Usalama kama wale watu watano niliowataja; kuna *Joint Intelligence Committee, Experts Committee*, ambayo ina Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Usalama wa Taifa na Mkuu wa Polisi. Hao ndio wataalam ambao wanakwenda kushauri hawa watu wengine.

Sasa leo tunapoanza kutengeneza kitu kingine hiki kitakuwa kwa kweli ni kitu cha Kitanzania tu siyo cha Kimataifa kuwa huo utaratibu umechukuliwa wapi. Naona uzoefu uliochukuliwa hapa ni kwamba, tunatengeneza kitu cha Muungano. Tuna *Executive President* ni lazima Rais apewe heshima yake ya kuwa *commander in chief* wa vitu ambavyo anaviongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ndiyo maana nilikuita wewe mtaalam wa hayo maneno kusudi uweze katuambia.

MHE. DKT. ANTHONY M. DIALLO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nipende kukushukuru sana na nishukuru kwa kuingia mwaka 2010. Natumia fursa hii, kuwatachia heri ya mwaka mpya wapiga kura wangu wote ambao hatujakutana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme kwamba, bahati nzuri mwenzangu amelizungumza na ameni-premty, lakini kuna maswali ambayo bado tungependa kujiuliza. Kwanza, hii sheria inakuja *in addition* kwa zile sheria tatu ambazo tunazijua; *Tanzania Intellegence Security Service Act, National Defense Act* na *Tanzania Police Force Ordinance*. Sheria hizi zote ukiacha nyingine, zinaweka vyombo ambavyo vinahusika na usalama. Sasa kwa mtazamo wangu, hivi vyombo vinaundwa kutokana na *Executive*; nilidhani hivi vitu vingetengenezwa *administratively*, Rais kama Rais anaweza kuweka utaratibu tu kuwe na chombo kama hicho; madaraka ya kufanya hivyo anayo.

Kinachofanyika sasa hivi ni kama Bunge hili Tukufu tukitaka *committee* tutunge sheria; ndiyo ninavyoliona hili. Sasa kuna mawili; tunaonekana Bunge tuko *idle* hatuna kazi nyingi, kwa hiyo, tunaanza kutunga Miswada tu ambapo mingine *actually inaduplicate* au inaweka mambo ambayo tayari yanachukuliwa yako kwenye mikono ya sheria nyingine. Mfano, majukumu yaliyotolewa ya Kamati za Wilaya kwanza niipongeze *Police Force*, ni mambo ambayo *Police Force already* mfano kwenye ulinzi shirikishi wanayafanya ni kazi yao.

Kwa hiyo, wangeweza ku-coordinate ulinzi watu wa Usalama nao watafundisha watu kutokana na bajeti zao na vyombo vingine vyote hata magereza *wikitaka* kuwafundisha wananchi wangeweza kuwafundisha. Sasa tunapounda chombo, kwanza, hiki ni chombo ambacho kinatokana na mhimili ule ule mmoja; sasa wanataka kuwe na sheria, ukiangalia sana na *Executive Powers* zao zile *actually zinakinzana* na mamlaka

kama alivyosema Mamlaka ya Rais ambayo anayo yanatosha na anaweza kuamulu kitu chochote kile. (*Makofi*)

Mimi naona hapo tuna tatizo, ukisoma Ripoti ya Septemba, 11 kwa nini kulitokea matatizo hata juzi yametokea walitaka kuteka ndege ya Kimarekani ni kwamba, unapokuwa na vyombo vingi unakuwa na tatizo la kila mmoja kujifanyia mambo. Sasa naona kinaundwa chombo ambacho bado hakitupi *guarantee* kwamba, ulinzi na usalama tunaoutegemea upewe kwa raia kulingana na Katiba, watakuwa wanautimiza. Mimi naona ni *cost centers* kwa sababu kwanza hawajatuambia *cost implication*. Kwa sababu hivyo vyombo vilikuwepo, walikuwa hawalipwi bali wanakunywa chai na maandazi pale wanakaa wanaondoka, sasa wanawekewa *high cost* ambayo ni *budget* kwa *tax payer*. Tunapigiwa kelele kwamba, *size* ya Serikali inakuwa kubwa sana, *as a result* tunatumia pesa nyngi sana kuendesha Serikali. Sasa hata majukumu yao ambayo yako Kikatiba tunaanza kuzalisha gharama ya kuyaendesha baadhi yao.

Sasa hawa wanafanya kazi gani, mnawawekea *cost* kwamba wakikusanyika mahala ni kama nilivyotoa mfano mzuri; Bunge tukikusanyika mahali tunazungumza mambo yetu ya Bunge tulipwe posho tena, kitu ambacho ni cha kawaida kwa watu wa nje wanaokuwa *involved*, lakini sisi kwa sisi nadhani mnajua dhahama tuliyoipata mwaka jana ya kuambiwa tunachukua mishahara miwili, tunafanya vitu gani. Kitu ambacho *actually* mpaka kesho mimi ninakipinga.

Suala hili linanisumbua sana hasa inapokuja *issue* ya *cost*, nadhani Sekretarieti hawakuliangalia vizuri. Tumezungumza juu ya asili, wamekekwa watu wengi; hivi kweli zitatunzwa siri za Serikali hapa? Tunajua kabisa kwamba kwenye *organization behavior* tunaambiwa *a size* ambayo inaweza kutunza siri ni watu *maximum seven* au wasizidi tisa, ukizidisha unakuwa ni mkutano wa hadhara. (*Makofi/Kicheko*)

Hii ni sawa sawa na kutuambia tutatunza siri, narudi namwambia mke wangu nilichokuwa ninakifanya, mke wangu na yeze ana marafiki zake; ninashaka sana hii haitakuwa tena *National Security* sijui *Commission Council*, utakuwa tu ni mkutano wa hadhara wa kuzungumzia mambo ya siri. Nina wasiwasi sana, tujaribu kuwa tunaangalia wenzetu wanapoanzisha *systems* huwa wanaangalia na ndio maana wanasema hata *cabinet* inapokuwa kubwa sana inakuwa kama mkutano wa hadhara, siri zote zitatoka.

Naomba tuwe waangalifu sana na mimi siungi mkono Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii ili nijaribu kuchangia yale ninayoona yanafaa kuyachangia katika Muswada huu.

Mimi natoa pongezi kwa kuuleta Muswada huu na nisije kusahau huko mwishoni, niseme mapema kwamba, naunga mkono hoja.

Pamoja na wachangiaji waliopita kuchangia vizuri na pengine kuweka mashaka kutokana na usiri wa utendaji wa chombo hiki, mimi nasema kwamba, kuletwa kwa sheria hii ni matokeo ya uzoefu wa kazi ambayo Mabaraza haya yamekuwa yakifanya. Mabaraza haya yapo wilayani na mikoani na wamekuwa wakifanya shughuli hii. Baada ya kuwa wameshazoea, wameona ni jambo linalowezekana sasa lifanywe kisheria, liingizwe katika sheria ili waweze kubanwa na kuongozwa kisheria suala la nani kuwa Mjumbe kama walivyopendekeza au nani kutokuwa Mjumbe. Vilevile sioni kama ni tatizo hawa kuwa Wajumbe, kwa sababu hawa ndio watu wa usalama; polisi ni watu wa uslama na unapomwona mtu kama IGP ameaminiwa mpaka kupewa cheo hicho ni mtu wa usalama. Watu wa Uhamiaji wa Taifa na Magereza kama hawaaminiki na kama siyo watanza siri; kwa nini wapewe yyeo vya juu kiasi hicho?

Hata Kamanda wa mkoa na wa wilaya wote wanafanya shughuli za usalama na wanatunza siri; kwa nini usiwaamini? Wajumbe wasiwe na wasiwasni na jambo hilo. Katika sheria hii, Kifungu cha 4(2)(i) wameandika kwamba: “*The Minister responsible for police and immigration,*” naona wamesahau *prisons*. Naomba hapo waongezee na *prisons* au waweke *Minister of Home Affairs*, badala ya kutaja *police, immigration, prisons*.

Ninaishukuru Serikali kwa *Schedule of Amendments* ilioletwa hivi sasa. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; niliongea naye kuhusiana na Wajumbe wale kwamba katika kifungu hicho cha 4(2) wameongeza “T” baada ya kifungu kidogo cha “S” kwa kumuweka *Commissioner of Immigration Services* kuwa ni Mjumbe Kitaifa; nashukuru sana kwa hilo.

Bado ninashauri wamuweke na *Principal Commissioner of Prisons* kwa sababu kama Mkoani huyu wa Magereza yupo na Wilayani wa Magereza yupo, hawa ni wadogo zake na huyu Mkuu wa Magereza Kitaifa ye ye hukumuweka hujamuamini kitu gani? Wadogo zake umewaweka ye ye hujamuweka, sioni kama mnamtenda haki; ni vizuri mkamuweka, kiprotokali kwanza ni kama haipo; kama ye ye hatakuwepo na wale wa Mkoani na Wilayani na wao waondoeni. Kwa hiyo, ninashauri kiongezeke kifungu kingine kidogo cha (l) awekwe *Principal Commissioner of Prisons* awe naye ni Mjumbe Kitaifa la sivyo kama hamumtaki huyo na wale wa chini wote waondoeni.

Ukitazama Kifungu cha 8(2)(I) na kifungu cha 10(I)(e) hapo ndipo ninapothibitisha kwamba, wale Wajumbe wa Mkoani kwa maana ya wa Magereza wapo lakini Kitaifa hayupo.

Niende Kifungu cha 4(5) ambacho kitashabihiana na Kifungu cha 4(6), Kifungu cha 6(2), kifungu cha 8(3) na kifungu cha 10(2). Katika utendaji wa Kamati anaweza akakaribishwa mtu ye yote wanayeona anaweza kwenda kutoa ushauri (*giving advice*). Nilikuwa nashauri liongezwe pia neno ambalo kama kuna mtu atalazimika kutoa habari

au labda ufanuzi fulani, neno hilo nalo liongezwe. Kama *giving advice* maana yake na hayo ninayoyasema nayo yapo, basi linatosheleza.

Kifungu cha 4(6), katika eneo la kupiga kura nilikuwa napenda ieleweke hiyo kura ni ya namna gani; ni ya siri; ya wazi; au ikibakia kama ilivyo wao watakuwa na uhuru wa kusema kura tunayoipiga ni ya siri au ni ya wazi? Nilikuwa nadhani ni vizuri ikawekwa kisheria kwamba, kura itakayopigwa pale itakuwa ni ya wazi au ya siri kutegemeana na jambo lenyewe. Hii ni kwa sababu Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoaa pengine ambaye ndiye Mwenyekiti, anaweza akalazimisha jambo fulani kwamba hili tunalipigia kura na wao kwa kumwogopa wakalipigia kura kutegemeana na Mwenyekiti wao anavyotaka. Baadaye kutaanza kuwa na uhasama mionganoni mwa Wajumbe wale kwamba, fulani katika kupiga ile kura ya wazi ye ye ndiye alikuwa kimbelembele kuikataa au akina fulani. Endapo itatajwa pale kwamba, kura itakayopigwa itakuwa ni ya wazi au ya siri, wakiamua kupiga kura za siri na jambo lile likapita au kukataliwa, hakutakuwa na uhasama wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magereza ni chombo ambacho kinawatunza watu ambao wameikosea jamii, watukutu na wakorofu ndiyo wanapelekwa wakapewe mafunzo au kuadabishwa. Magereza ni kazi ngumu, kukaa na binadamu mwenzako ambaye huko kwenye jamii ameshindikana ninyi ndiyo mnaletewa kumtunza na wale nao wanaokwenda kule ni wahalifu na wana mambo mengi wanayoyajua na mengine ni makubwa na ya siri kutokana na kazi walizokuwa wanazifanya huko za uhalifu wanatoa siri kwa Maafisa wa Magereza, labda Wakuu wa Magereza na kadhalika.

Kwenye Baraza hili kule Mkoani na Wilayani mmekwishawaweka hawa Wakuu kuingiza kwenye Baraza hilo, sina tatizo nao. Sasa pale Taifani inaonekana kama vile yule Mkuu wake hajui chochote na kwa hiyo kuingiza kwenye Taifa hakuna haja.

Namalizia kwa kushawishi Mkuu wa Magereza Kitaifa aingizwe kwenye Kamati ya Kitaifa.

Mimi ninaunga mkono hoja. Baada ya marekebisho hayo kufanyika, ninaamini Serikali itakuwa imeona umuhimu wa hilo na itarekebisha na moja kwa moja naomba nikae huku nikiwa nimeunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa William Shellukindo, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa. Nimepata tena maombi mengine kutoka kwa Mheshimiwa John S. Malecela.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa.

Kwanza kabisa, naomba kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Mimi niliufulitalia Muswada huu, naona una mengi ya kuboresha; ule wa kwanza uliokuja

ulikuwa mrefu sana na uliweka mambo mengine mengi tu ambayo katika masuala ya usalama kwa kweli hayakuhitajika; na katika huu naona umeelekeea elekea kukidhi yale ambayo tunadhani yangekuwemo. Sasa naipongeza sana Serikali, pamoja na Waziri mwenye jukumu hili, kwa kuhakikisha kwamba, kunakuwa na chombo ambacho kinamsaidia Rais katika kutekeleza jukumu lake la Amiri Jeshi Mkuu.

Kabla sijaingia kwenye kuangalia yale maeneo ambayo nataka kuchangia, nilitaka tu nimtake Mwanasheria Mkuu; kumekuwa na utata hapa wa kutumia alama ambazo Kimataifa zinazokubalika. Kuna wakati mmoja nilizungumza hapa nikaambiwa ndiyo utaratibu wa kutunga Sheria; utaratibu wa kutunga Sheria hauwezi kuondokana na vitu vingine ambavyo vinakubalika Kimataifa; kuna alama ambazo zinakubalika huwezi kuweka koma mahali ambapo palitakiwa kuwekwa *full stop* na huwezi kuweka mstari mahali ambapo ultakiwa uweke *column*. Sasa Mwanasheria Mkuu mimi nimekuelewa sana kwenye mambo yako haya ya kwenda na ufanisi.

Katika sehemu ya pili ukurasa wa nne, pale ambapo inaanizishwa ile *Council*, *Section 4(2)* inasema: “*The Council shall consist of the following members,*” kwa mujibu wa tafsiri hako kamstari kwenye Sheria mnakaita nini; hakana jina? Sasa naomba hapo iwekwe *colon* kwa sababu *colon* zinawekwa mahali ambapo kuna orodha ambayo inafuata. Ninaomba tukubaliane hiyo na mahali popote ambapo kuna orodha hako kamstari kaondolewe; kamstari kako kwenye alama kanaitwa *hyphen* na kanatumika kuunganisha maneno mawili. Kwa hiyo, hapa tunawachanganya hata vijana wetu walioko shulen, wakisoma watashangaa sana kwamba hivi hili Bunge linatoa wapi haya mambo mengine ambayo linaweka. Hilo ningependa baadaye tukubaliane ili Miswada inayokuja iende na hizi alama ambazo zinakubalika kama *full stop*, *semi colon*, *hyphen* na kadhalika, zikae vizuri ndiyo tuonekana kwamba tunakwenda vizuri.

La pili, naungana kabisa na wenzangu waliotangulia kuzungumza na hasa Jenerali Mstaafu Ngwili; Baraza la Usalama la Taifa siyo kongamano, kwa hiyo, tusigeuze pale kama ni kongamano, hapana. Hapo ni mahali pa uamuzi; tuna Amiri Jeshi Mkuu ndiye mwenye kutakiwa kutoa uamuzi. Kwa hiyo, anataka apate muafaka katika hali yetu ya Muungano kwa mfano kama hivyo akae na wenzake wa ngazi za juu waseme tuna hali hii, tumpata ushauri ufuatao kutoka kwa watekelezaji na sasa tukubaliane kufanya hili.

Baada ya kufanya hayo, hao wengine wanakwenda kuwa *briefed* kwamba, kuna kazi hapa ya kufanya; sasa tusifanye mahali pa *ku-negotiate* watakuwa wanamuingilia Rais kwenye madaraka yake. Rais anapewa ushauri, sasa hii habari ya kupiga kura hapa kwenye maamuzi, inanipa taabu kidogo; hivi kwenye Baraza la Mawaziri mnapiga kura? Hapana, mnazungumza mnafikia muafaka mnamwachia Rais akaseme. Sasa kwa nini tunaingiza vitu vingine hivi na vilevile tupambanue kati ya maeneo ya kutoa uamuzi na maeneo ya utekelezaji.

Kwa mfano, unahitaji uamuzi kuhusu hali ya maafa, taarifa zimeletwa, Waziri Mkuu ndiye ameziunganisha hizo. Sasa kama kuna uamuzi unaotakiwa kutolewa, tuna Serikali mbili; hao Viongozi wa juu kama alivyosema Jenerali Ngwilizi, Marais hawa wawili, Mawaziri Wakuu wawili, hao wengine wanakaribishwa kwamba hebu njooni

tuangalie hili suala lakini uamuzi uachwe katika ngazi hiyo. Kwa hiyo, katika hali hiyo hii orodha yote nimehesabu wako 20, hawa kama alivyosema Jenerali Ngwilizi ni sawasawa na *cabinet* ya pili. Sasa tusije kufika mahali tukaigawa na *cabinet* vilevile na kusema kwamba, aah, bwana kuna watoto wa watu wametoa uamuzi sisi tutekeleze tu, hapana! Twende pamoja, Rais ashauriwe atoe uamuzi watekelezaji waelezwe kwa kutegemeana na walivyoshauri.

Kwa hiyo, kwa mfano, hawa wakuu wa vyombo vyaa ulinzi na usalama hawana haja ya kukaa hapa; hawa ndiyo wanaokuja kueleza kwamba tuna hali hii tumeitafakari, kwa hiyo, tunataka kufanya kazi. Hebu niulize; hivi Mwalimu wakati anaamua tuingie kwenye vita kongamano gani lilikaa? Hapana! Walifanya ushauriano kwenye ngazi hizo halafu wakaingia kazini ndiyo wakasema hali iko hivi, uwezo tunao, nia tunayo tunakwenda kazini. Sasa hii ya kuanza kupiga kura inatupa matatizo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama orodha hii itabaki katika kifungu cha (4) kama ilivyo, ninaomba kuanzia pale (g) ile orodha ya wale Wajumbe walioko kama itabaki basi kuanzia (g) mpaka (l) yale majina ya zile Wizara yaandikwe kwa herufi kubwa, hapa yako kwenye herufi ndogo. Sijui kama mtoa hoja ananielewa hapa? Kwa mfano, *Minister responsible for defence* imeandikwa kwa herufi ndogo, *Minister for Immigration* imeandikwa kwa herufi ndogo, *Minister for Finance* imeandikwa kwa herufi ndogo, *Governance* hiyo ya mwenyewe herufi ndogo, *Legal Affairs* herufi ndogo, naomba ziwe herufi kubwa maana hii Sheria itatoka tusije tukahesabika kama watu ambaa tunaangalia mambo ovyo ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo madogo madogo ambayo kwa sababu jedwali la marekebisho limekuja tumepewa sasa hivi na vilevile nimeangalia haya mambo ambayo nimeona niyaweke sawa hayamo, basi nitakwenda nayo tukifika kwenye Kamati ya Bunge Zima nitasimama ku-*move* hizo *amendments*. Nafurahi sana kwamba, kwa mfano, marekebisho yaliyopo katika kifungu B wanazungumzia habari ya *semicolon*, koma na zile nilizosema ziwekwe ziingie katika hiyo, wakati ukifika nitasimama niziweke sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 4(5), ukurasa wa 5, nilikuwa natatizo kidogo pale wanaposema kwamba: *The Council may invite any person in its meeting* iwe meetings siyo mkutano mmoja. Kwa hiyo, kila mahali wanapoandika *meeting* ni meetings siyo mkutano mmoja ule. Vilevile nitapenda *Attorney General* tukubaliane, kwa mfano, sentensi hiyo ni vizuri zaidi tuandike *The Council may invite any person in its meetings* au to its meetings; hebu tukubaliane hapo ni ipi labda utakayoiona wewe ni nzuri zaidi tuitumie, mimi nadhani to its meetings ikanaa vizuri sana.

Eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni Kifungu cha 6(1)(a); ninaomba ile *head* pale inaposema *The Chief Secretary who shall be the head and the Coordinator* kisiwekwe kichwa cha mtu bali iwekwe *head* ya kiongozi, imeandikiwa kwa herufi ndogo.

Katika ukurasa wa 7 Kifungu cha (7)(1) ile (d) ningeomba turekebishe pale panaposema *keep and maintain records and control confidentiality of all documents*

relating to the Council activities. Hiyo Council iwekwe apostrophe na iwe Council's activities na hiyo "s" iingie hapo.

Tukija vilevile kwenye kifungu kidogo cha (2) katika sehemu hiyo hiyo pale inaposema *the Secretariat may co-opt any person during its meeting* siyo mukutano mmoja tu tutawabana hawa kwamba wameshafanya mukutano mmoja kwa hiyo wasiendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo niliona tuliweke sawasawa ni katika ukurasa wa 9, bahati nzuri wameleta marekebisho hapo nimekubalana nayo na mimi nimerekebisha huku kwangu.

Katika ukurasa wa 10, Kifungu cha (3) kinachoanza na *Where the District has more than one Council*, nayo tuibadilishe *all Directors* kwa sababu mmeshasahihisha kwamba ile *Executive* iondoke, kwa hiyo na hapa tuondoe ile *Executive Directors* iwe *all Directors of the Local Government Authorities* na hizo ziwe *capital tafadhali*.

Katika ukurasa wa 11, kifungu cha 14(2) ile sentensi ya tatu ni kunyoosha tu kile kiingereza pale kwamba, *the defence and security committees*, badala ya *considers tuseme consider necessary*, maana yake tumetumia wingi pale.

Pia Kifungu cha 14(3) kilichoko ukurasa wa 12, ilipoandikwa *without prejudice to subsection (2), the Council, the Regional Security Committees and the District Security Committee*, iwe *Committees* iwiiane na hizo za Mkoani.

Katika ukurasa wa 13, Kifungu cha (19)(d)(ii) inaposema; *inserting the words "the Council" immediately after the words "United Republic" appearing in fourth line* ingekuwa *in the fourth line*, kwa hiyo, ingeingizwa *the pale*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jedwali ukurasa wa 16, nilizingatia lile rekebisho katika kifungu cha 3(ii), lakini kifungu cha (i) ningeomba *Attorney General* tukubaliane kidogo, tukiboreshe tuseme *The Councils shall meet at least quarterly and at such times; nadhani ingekuwa at such other times as may be necessary*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ya kwangu yalikuwa haya tu na kwa hiyo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Willibroad Slaa, atafuatiwa na Mheshimiwa John Malecela na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ajiandae.

MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kidogo Muswada huu muhimu. Masuala ya usalama na ulinzi katika Taifa lolote ndiyo uhai wa nchi na yasipoandaliwa vizuri, unaweza kualika matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuangalia Sheria yetu; katika tafsiri imetenganisha au imeweka tahadhari katika *application* sehemu ya 2(2) kwamba, inatenganisha *operational level*, yaani katika utendaji nadhani kama tafsiri ni sahihi pamoja na mambo mengine yote isipokuwa kwa yale ambayo yanahusika na maslahi ya Taifa moja kwa moja.

Nianze kwa kusema kwamba, kinachotuongoza katika kujadili maslahi ya Taifa katika usalama na ulinzi ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 33, ambayo iko wazi kabisa na inaeleza kwamba; kutakuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na jukumu lake limeelezwa katika Ibara ndogo ya (2), atakuwa ni Mkuu wa Nchi, atakuwa ni Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu.

Tunachozungumzia hapa ni kisehemu hiki cha Amiri Jeshi Mkuu. Sehemu ya Amiri Jeshi Mkuu huwa haigawanyiki ni moja tu; Jeshi huwezi kuwa na Mamlaka mbili zinazotoa maagizo. Sasa cha kwanza katika Sheria hii ambacho tunakiona katika kifungu cha 6 ambacho baadaye kitatafsiri Ibara ya 4; Kifungu cha 6 kinalezea jinsi utendaji kazi wa Baraza na muundo utakavyokuwa (*The decision of the Council shall be by vote*). Sheria inayotumia neno *shall*, haitumii neno *may*, inatumia *shall* kwamba ni lazima katika maamuzi ya chombo hiki kutakuwa na kupiga kura. Ingekuwa *may* angalau kungekuwa na uhuru, labda mazingira fulani fulani. Neno *shall* likitumika katika Sheria maana yake ni lazima katika maamuzi itakuwa ni uamuzi wa *majority*, yaani anatamka *majority* maana yake Amiri Jeshi Mkuu, katika suala la ulinzi na usalama unam-subject unamuweka chini ya uamuzi wa hawa wote waliotajwa sijui wapo wangapi, hapa umeorodheshwa mlolongo mzima ambaao ni sawa na kongamano, ndiyo wanapiga kura kumzidi Mwenyekiti Amiri Jeshi Mkuu; waamue kwa wingi juu ya jambo la ulinzi na usalama kwa mtu ambaye Taifa zima limemuamini na kumpa kura kwamba, huyu ndiye atakuwa Kiongozi wetu wa nchi. Mimi ninavyoona jambo hili linakwenda kinyume na Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge halipaswi kutunga Sheria inayokwenda kinyume na Katiba; ni lazima Bunge lilinde Katiba kwamba Kiongozi huyu tumempa mamlaka na mamlaka ya Rais hayagawanyiki. Mheshimiwa Rais wetu ametumia neno moja zuri sana kwamba, hana ubia na mtu yejote; huwezi kumpa Rais ubia kwa kupiga kura na watu ambaao anapaswa kuwaagiza wakimbie kulinda Taifa. *Commander in Chief* akishaagiza wale *Defence Forces* wote wanapaswa kukimbia kutekeleza na amri ya Amiri Jeshi unaitekeleza kabla ya kuuliza. Sasa unaanza kuuliza kwa kupiga kura badala ya kutekeleza agizo la *Commander in Chief!* Nadhani tunakwenda kinyume na dhana nzima tunayopaswa kulinda katika ulinzi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kuyaeleza haya kwa sababu mara ya mwisho Bunge liliurudisha Muswada huu Serikalini ili haya yote yaondolewe, hayakuondolewa! Kama yaliondolewa basi yamedonyolewa donyolewa, wamefanya *operation* wameondoa yale mengine lakini wakasahau hili la msingi; na hili la msingi ndilo lililofanya Muswada huu ukataliwe kwa sababu ulikuwa unakiuka mambo ya msingi; ni kitu gani zaidi tulichokataa kama siyo haya wakati ule?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 34(4) inaelekeza madaraka ya Rais yanatumikaje, bila ya kuathiri masharti; kwa kibali chako nankuu: "Bila ya kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatakelezwa ama na Rais mwenyewe moja kwa moja au kwa kukasimu madaraka hayo kwa watu wengine."

Madaraka ya Amiri Jeshi huwa hayakasimiwi, sijaona *instrument* yoyote katika Sheria au mahali pengine popote Rais akikasimu madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu, madaraka mengine yote yanakasimiwa kwa Rais kutoa *instrument* ya kukasimu madaraka na wale wengine wote waliopewa kazi; Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya haya yamekasimiwa, wanafanya kazi kwa niaba ya Rais lakini hata siku moja hawaendi kufanya majukumu mengine ya Rais.

Ifahamike kwamba, masharti katika Ibara hii hayatahesabika kwamba yanahamishia kwa Rais madaraka yoyote kisheria yaliyowekwa na Sheria mikononi mwa mtu au Mamlaka yoyote ambayo siyo Rais. Sheria imeweka Mamlaka kwa kila mmoja, lakini kwa Sheria hii hapa tunahamisha yale ya Rais ambayo kimsingi Katiba yenye haikutaka kuyahamisha; ni jambo ambalo ninaliona ni la hatari kweli kweli.

Ibara ya 33 inatambua kwamba, Rais wetu ni *Executive President*. Kabla ya kubadilisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano, huwezi kumwondoa Rais kuwa *Executive President* kwa Sheria. Sheria inapaswa kutekeleza yale ambayo Katiba inalinda, tunganeza na kubadilisha Katiba, leo tunaanza kuondoa *Executive Presidency*; hapo tungelianza kuaondoa Mamlaka hayo, tungekuwa na Waziri Mkuu ambaye naye ana majukumu yake akawa ni mshauri, kwa maana hiyo unamuundia Baraza la Ushauri; hapo ningelewa kwamba, unaanza sasa kutengeneza chombo kingine, lakini Rais yule yule *Executive President*, unamtengenezea Sheria halafu Mamlaka yake anawenza kunyang'anywa kwa njia ya kupiga kura; ni jambo la hatari sana katika nchi yoyote ile. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusema kwamba, hapa ninaona kitu ambacho hakikuandaliwa vizuri. Ukirudi katika Ibara za 145 na 146 za Katiba, ambazo ziko *very clear*; Ibara ya 146 inatamka kwamba, madhumuni ya kuwepo Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi na vyombo vya Serikali za Mitaa vitakuwa na mamlaka ya ushiriki kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji katika sehemu zao na nchini kote kwa ujumla.

Sasa kumekuwa na *tendency* katika nchi yetu, kupeleka Serikali Kuu ambayo mwanzoni tuliiweka mpaka kwenye mkoaa, tukajua mpaka wa Serikali Kuu ni mkoani ndiyo mwisho wa Serikali Kuu. Mwaka 99 tulipotunga Sheria Namba 19, tukaenda hatua mbele tukamuweka Mkuu wa Wilaya ambaye mwanzoni alikuwa kama Mratibu na kadhalika, tukaenda kumsogeza akawa kama sehemu ya Rais kule chini, lakini Katiba yetu inatamka dhahiri katika Ibara ya 146(2), inaweka wazi bila ya kuathiri maelezo ya jumla yaliyomo katika Ibara ndogo ya kwanza ya Ibara hii chini kila chombo cha Serikali za Mitaa kwa kuzingatia masharti ya Sheria iliyokianzisha kitatusika na shughuli zifuatazo:-

Kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa katika eneo lake; na kuhakikisha utekelezaji na ulinzi wa wananchi. Sasa unaunda chombo hiki tena cha ulinzi na usalama chini ya chombo kingine amba ni mkondo mwingine, maana yake unaondoa ile dhana nzima ya *D by D*, ambayo Serikali yetu kwa zaidi ya miaka 10 na kitu sasa tumekuwa tukijenga. Unajenga dhana moja halafu kwa ghafla tu unafuta yale yote uliyokuwa umeyafanya, tumetumia mabilioni ya fedha katika kujenga *D by D*, wananchi wanapewa mamlaka badala ya kuongeza nguvu. Mkurugenzi awe ndiyo chombo cha kusimamia ulinzi amba anapewa mamlaka hayo na Katiba, tunaondoa tunahamisha na kupeleka kwa Mkuu wa Wilaya; tunakiuka Katiba tuliojiwekea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya, nadhani sihitaji kuendelea. Nitaomba tu mchango wangu uende pamoja na kutumia kifungu cha 69 cha Kanuni kinachosomeka kama ifuatavyo; naomba ninukuu: “Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba mjadala huu sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na piaatalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala huu uahirishwe.”

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitimize masharti ya Kanuni kwa sababu ninafikiri kwamba, Muswada huu haujaiva kwa kuwa unaashiria kukiuka Katiba ya Jamhuri na katika jambo zito la ulinzi na usalama wa nchi yetu. Katika jambo zito kama hili, Bunge litakapokuwa limeupitisha na Katiba inatukataza kuitisha jambo lolote ambalo halijaiva, basi Bunge hilo litakuwa siyo makini. Bunge letu hili ni makini, tunapaswa kulinda maslahi ya Taifa na tunapaswa kuangalia tusigonganishe Sheria zetu; ni lazima Bunge hili sasa niliombe na niwashawishi wenzangu mjadala uaihirishwe mpaka Serikali itakaporekebisha vifungu hivi muhimu vinavyo kukiuka Katiba ya Nchi yetu na kutuwekea jambo ambalo ni halali na ambalo linaweza kulinda ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa namwita msemaji anayefuata Mheshimiwa John Malecela.

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia ningependa nichukue nafasi hii nikiwa ninachangia kwa mara ya kwanza katika Bunge hili tangu limeanza mwaka huu, nataka niwatakie Wabunge wote heri ya mwaka mpya na hasa niongezee kwamba, ninawatakia ninyi nyote mkafanye kazi vizuri kwenye Majimbo yenu ili Bunge lijalo tukutane tena. (*Makofî*)

Baada ya kusema hayo, ningependa nieleweke kwamba, ninapochangia juu ya Muswada huu, ninataka tufikirie maana hiki ndiyo kiini cha nchi. Ulinzi wa nchi ndiyo jambo muhimu, jambo la maana na ni jambo ambalo halitaki liwe na utata mahali popote. (*Makofî*)

Kwa hiyo, maneno nitakayoyasema siyo kana kwamba mimi ninaipinga Serikali, lakini nia yangu ni kwamba, tuunde vyombo ambavyo kweli vinaweza vikasimamia uhuru wa nchi yetu. Kwa nini tunampa Rais madaraka makubwa na tunasema yeye ni Amiri Jeshi Mkuu, ambaye anawenza kuamuru kwamba Jeshi fulani liende mahali fulani bila utata wowote. Kwa hili tunasema kwamba, mpaka kwanza kile chombo kikakae. Nitoe mfano; ni kweli tunasema kwamba chombo hiki hakitakuwa *Executive* lakini ukiangalia kwenye Muswada unakuta kinakuwa kwa sababu kuna ibara inayosema wakishapiga kura, chombo hiki kikishapiga kura, maamuzi yake ni lazima yatekelezwe. Sasa hapo tunasema chombo siyo *Executive?* (*Makofi*)

Kwa upande mwingine, tunawapa madaraka ya kupiga kura. Mkiangalia katika ibara ya 5(d) na (e), unakuta mambo haya yapo. Ningependa tu niseme ninakubaliana na yote ambayo Bwana General Ngwilizi ameyasema. Sasa nije moja moja kwenye hoja; kwanza, nataka niseme chombo hiki ni kikubwa mno na jinsi unavyokuwa katika mambo ya ulinzi na usalama, jinsi unavyokuwa na kitu kikubwa, ndivyo kinavyozidi kuwa kigumu kuki-*control*.

Mara ngapi tunakaa kwenye Kamati zetu tunasema suala hili ni siri keshounalikuta kwenye magazeti! Mnakaa mnazungumza mnasema jamani yaishie humu humu, kesho unakuta *word by word* ni nani aliyasema haya? Sasa hiki ni chombo kitakachokuwa kinashughulika na usalama wa Taifa halafu kinakuwa kikubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki ndicho kitakachokuwa kina-*control* Jeshi, Polisi, Usalama wa Taifa, halafu tunasema wao ndio watakuwa wana-*analyse* na *ku-evaluate* mahali pengine na ndiyo watakuwa wanaamua *deployment*. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, tukija kwenye neno *deployment* maana yake ni kwamba, chombo hiki kinaweza kikaamua kwamba, sasa *battalion* fulani iende mahali fulani na ile nyininge iende mahali fulani. Sasa sijui kama kweli tutakuwa tunasema tuna usalama wa Taifa.

Ndugu zangu tungakuwa na chombo hiki tungekwenda Comoro? Tungekwenda Comoro kwa wakati unaotakiwa na kwa muda unaotakiwa na tukafanya kama tulivyofanya au chombo hiki hiki kingetuwezesha kusaidia kwa haraka Seychelles. Mheshimiwa General Ngwilizi anafahamu sana maamuzi yalivyokuwa wakati jeshi letu linakwenda kusaidia Seychelles wakati walipokuwa wamevamiwa na makaburu.

Ndugu zangu nataka niwarudishe tena kwenye madaraka ya Rais. Jamani kuna madaraka ya Rais ambayo kwa hili nakubaliana na Mheshimiwa Dkt. Slaa, ambayo hayagawanyiki. Nasema hivyo kwa sababu hapa tunachozungumza ni usalama wa nchi. Kuna wakati mmoja Marehemu Mwalimu Nyerere, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi; alikuwa amesafiri nje ya nchi na aliyezesa ameshika madaraka kama *Care Taker* alikuwa Mheshimiwa Aboud Jumbe. Mheshimiwa Aboud Jumbe akasaini *Detention Order* na akatiwa ndani, lakini *lawyers* wa yule aliywewka *detention* wakaenda kui-*challenge detention* katika Mahakama ya Arusha na nakumbuka wakati huo Jaji alikuwa Jaji Mweisumo, ambaye baadaye alikuja kuwa Mbunge humu humu

ndani; na baadaye Mahakama ya Arusha ikaamua kwamba ingawa Rais aliye kuwa hayupo ameacha madaraka ya mtu kukaimu, huyu anayekaimu hana madaraka fulani fulani pamoja na kutokuwa na madaraka ya *detention*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, yule bwana akaachiwa na nadhani mpaka sasa tunayo hiyo *presidency* kwamba, mtu akikaimu hana madaraka ya kumtia mtu ndani. Hayo ni madaraka ya Rais peke yake. Kwa hiyo, mimi ningesema kwamba, Sheria hii ina nia nzuri sana na inaitaka nchi yetu iwe katika ulinzi mzuri, lakini ninasema pengine imeletwa kwa wakati ambao siyo muafaka. (*Makofi*)

Haya mambo ambayo tumeyasema humu, mimi sitaki kwenda kule kwenye Mikoa na Wilaya, zile za Mikoa na Wilaya ni sawa sawa, lakini huku juu ambako kunahitaji maamuzi ya haraka. Mwalimu alipoamua kwamba, twende Kagera tuvuke mpaka tumfuate Iddi Amin, yalikuwa ni maamuzi makubwa. Sasa leo tuangalie katika nchi za wenzetu; maana sisi Tanzania hatuko katika kisiwa; wapi umekuta kuna Rais wa kuchaguliwa anakuwa na Kamati kubwa namna hii ya kumshauri mambo ya kivita. (*Kicheko*)

Pamoja na ubabe wake lakini Bush alipokuwa anaamua kwamba, majeshi yaende Iraq, hakuwa na dude kubwa la kumshauri kama hivi. Obama kaja juzi, pamoja na wote kumsifu na nini, lakini na yeye bado anaamua vile vile. Jamani madaraka makubwa kama haya ya nchi tuyaa che yabaki mikononi mwa Rais, laa sivyo, tutafika mahali hata mtu wa Usalama wa Taifa kuteuliwa litakuwa sasa ni suala la kampeni, apite kwa huyu, apite kwa yule, hatutakuwa na usalama unaoaminika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningeomba kwamba, Muswada huu si wakati wake ukaangaliwe tena; na tunasema kutoka moyoni, kwa nia njema ukaangaliwe tena, uletwe wakati unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa mtoha hoja.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Umeninyima nafasi yangu?

NAIBU SPIKA: Ndiyo, mimi ninaendesa Bunge kufuatana na ninavyoona.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote, kwa kuleta Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa usalama na ulinzi wa Taifa letu. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu utakuwa na maana kwa Taifa kama mambo yafuatayo yatazingatiwa:-

(i) Uteuzi wa Wajumbe katika nyadhifa zao uzingatie pia kuwa hawa wanaoteuliwa wana msimamo gani na wana uwezo kiasi gani kulinda usiri wa mambo yanayojadiliwa ndani ya vikao.

(ii) Uwezo wa Wajumbe kutambua hali ya mabadiliko ya nchi na watu wake, wakizingatia nidhamu na utandawazi unavyomega mshikamano mionganoni mwa wananchi.

(iii) Majukumu ya chombo hiki lazima yawe tofauti na majukumu ya kabla na baada ya Uhuru. Lazima yawe tofauti na kipindi cha mfumo wa vyama vingi ulipoanza 1992/93. Sasa tuko katika kipindi cha vyama vyenyewe kuvurugana na kuashiria vurugu katika nchi.

(iv) Kuwa macho na kutumia wananchi waaminifu ili kutoa taarifa sahihi juu ya hali ya usalama wa Taifa. Magazeti yatumike kwa kuchambua hali ya nchi na kuwatumia pia wahariri na vyombo hivi ili wasaidie kutoa taarifa mbazo haziwezi kuhatarisha usalama wa Taifa.

(v) Ajira ya Watumishi wa Idara hii iendelee kufanyika kwa uangalifu sana. Pia maslahi ya Watumishi hawa iwe ya kuwafanya wawe watumishi waaminifu na wenye ari ya kutekeleza majukumu yao vizuri.

(vi) Matumizi ya *Informers* yafanyike kwa kasi zaidi na yajumuishet hata wale tunaowaona ni wakorofu katika jamii ili tuwaweke karibu na vyombo hivi vya usalama.

(vii) Kuongeza uwezo wa watumishi kujua majirani na mataifa mengine yanafanya nini na mbinu zipi zinaendelea kutumika katika kutukwamisha kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, lakini naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Karume, kwa kukubali muafaka wa kuunda Serikali ya Mseto katika Serikali ijayo baada ya Uchaguzi wa 2010. Tunawaombea wenzetu wa Zanzibar wamalize mambo yao kwa usalama ili maisha yao yaendelee kuwa ya salama kwa sasa na miaka mmingi ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Wajibu wa kila Mtanzania kuungana na hoja hii, kwa sababu ulinzi na usalama wa Taifa ni jukumu la kila Mtanzania. Lipo tatizo kubwa ambalo linawakumba Watanzania wengi kuhusu suala la usalama wa nchi kuwa uko chini ya vyombo vya ulinzi na usalama tu na hasa chombo cha usalama. Ni makosa makubwa. Hali hii inajidhihirisha kutokana na watu kutokuwa tayari kutoa kwa hiari taarifa ambazo zinahatarisha usalama wa Taifa kwa chombo cha dola cha usalama.

Ni wajibu wa kila mwananchi kuwa mstari wa mbele katika kuwa makini kwa kutambua vitendo na watu wabaya ambao wanakwenda kinyume na ulinzi na usalama.

Hata hivyo, ni muda muafaka sasa Sheria ingeweka adhabu ya kutosha kwa wale wote wanaotumia jina la vyombo nya ulinzi na usalama ili kujinufaisha ama kutenda maovu. Watu wa aina hiyo wanachangia kwa kiasi kikubwa kuchafua maana halisi ya vyombo. Sheria izingatie na kuchukua hatua kali dhidi ya watu wa aina hiyo na hiyo iende sambamba na wananchi kutokuwa na chuki na kuwaogopa watendaji wa vyombo hivyo.

Baada ya hayo, napenda kuupongeza Muswada huu kwa asilimia mia moja. Vyombo vyote nya ulinzi na usalama viwezeshe kifedha ili kufanya kazi zao vizuri.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka.

Suala la usalama wa Taifa ni muhimu na nyeti katika kila Taifa Huru. Bila usalama wa Taifa kwa mapana yake, nchi haiwezi kuwa na uhuru wake kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muundo wa Kamati za Usalama wa Taifa, nashauri uwepo wa Maofisa wa Idara ya Magereza hususan katika ngazi za Mkoa na Wilaya. Katika ngazi hii ya Mkoa na Wilaya pia si vibaya kama wangejumuishwa Viongozi wa Madhehebu mbalimbali ya Kidini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa katuongoza vizuri na hivyo kuifanya nchi yetu kuwa salama.

Naipongeza Ofisi yake na wote waliopo katika Ofisi ya Rais (Utawala Bora), bila kumsahau Waziri wake, Mheshimiwa Sophia Simba.

Ushauri wangu ni wa kawaida, kuwa na sheria ni kitu kimoja na kuitumia sheria vizuri ni sehemu ya pili. Tatizo kubwa nimeliona katika mazingira ya siku hizi, neno usiri katika mambo muhimu umezungua kidogo lakini pia naona kama vyombo nyeti katika kuwa karibu na sisi wananchi, tumejikuta tumechukua nafasi zenu na kuwajengea taswira ya kuegemea katika baadhi ya makundi na hivyo kuwafanya kutokuwa na nguvu zinazojitegemea katika ufuutiliaji na maamuzi. Nafahamu kazi ya usalama ni ngumu na nyeti na pengine kufanya kazi bila mapumziko.

Nazidi kuwaombea na kuwaomba kuzingatia ushauri wa msingi ambao Waheshimiwa Wabunge, Wataalam wa eneo hili wanavyochangia.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Serikali kwa wazo la kuunda Baraza hili la Kitaifa; ni jambo jema. Uundwaji wa Baraza na Matawi yake kufika hadi ngazi za chini ni kuwasogelea zaidi wananchi, jambo linaloendana na dhana ya ulinzi shirikishi. Pamoja na ubora wa Muswada huu, ninashauri yafuatayo:-

(i) Baraza liende chini zaidi hadi ngazi ya Tarafa likiongozwa na Afisa Tarafa.

(ii) Katika Baraza ngazi ya Tarafa sungusungu wawakilishwe.

(iii) Marekebisho mbalimbali yaliyoanzisha Mgambo na Jeshi la Polisi yafanywe ili uhusiano dhahiri kati ya majeshi hayo na sungusungu uonekane. Hii ni kwa sababu sungusungu wako karibu zaidi na jamii kuliko vikosi hivyo viwili. Hivyo, itakuwa rahisi zaidi kutumia Jeshi hili la Wananchi wenyewe kutambua na kuongoza matatizo ya kiusalama kupitia sungusungu iwapo watatambuliwa kisheria na wao kujitambua kuwa nao kisheria ni sehemu ya vyombo nya usalama.

(iv) Ukubwa wa Baraza upunguzwe na kura za maamuzi zisiwepo. Kura zaweza kukwaza mambo mengine nyeti kwa Taifa.

Pamoja na maoni hayo, ninatanguliza pungezi zangu kwa serikali, nikilitakia Baraza hili utendaji mwema. Ninaunga mkono hoja hii.

MHE. DKT. JAMES A. MSEKELA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia Muswada na ninaamini kwamba, unahitaji kujadiliwa kwa kina zaidi nje ya Bunge. Katika kuujadili ni vyema kwanza madaraka ya Rais yakahifadhiwa katika ukamilifu wake. Vilevile hivi sasa kuna sheria kadhaa ambazo bila kuweka shinikizo laini au gumu ama la aina yoyote nyingine, zinatekeleza majukumu haya yanayodhamiriwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwani kumeonekana udhaifu gani kiasi cha kutaka kuunda Baraza? Je, inawezekana udhaifu ulikuwa ni wa kusimamia Sheria hizo ama baada ya vyombo husika kufikia ukomo wake wa kimadaraka kwa mujibu wa Sheria sasa imeonekana haja ya kuimarisha zaidi Utawala wa Sheria (Utawala Bora) kwa kutaka kuongeza nguvu ya usimamizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna mambo mazito ya kurejea kwa kina kabla ya kusonga mbele na Muswada huu. Muda unaohitajika kufanya hivyo ni mwingi na utawezekana kupatikana kwenye Kamati ya Bunge (nje ya Bunge).

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hoja ya msingi ni kuharakisha Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa na Wilaya, ambazo kwa muda mrefu zimekuwepo kinyume cha Sheria, hivyo umepelekea kuletwa kwa Muswada huu.

Kwa bahati mbaya, Muswada huu kwa nia hiyo unapunguza mamlaka na madaraka ya Rais, kitu ambacho ni kinyume na matakwa ya Katiba yetu.

Kwa maoni yangu, Muswada huu unapaswa kuandikwa upya na kupitiwa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

MHE. MUSSA AZAN ZUNGU: Naunga hoja.

Naomba nipewe maelezo kwa nini Muswada huu hauzungumzii suala la Mshauri wa Usalama kwa Rais (*National Security Advisor*)?

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, namwita mtoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa tena. Vilevile ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada huu kwa umakini na kwa uwezo mkubwa.

Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechangia kwa maandishi anaanzia Mwenyekiti wa Kamati ambayo iliuchambua Muswada huu, Mheshimiwa George Malima Lubele na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa wengine waliochangia ni Mheshimiwa General Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Dkt. Anthony Diallo, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa na Mheshimiwa John Samwel Malecela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwataje waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, Mheshimiwa Azan Zungu, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Dkt. James Musekela, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. (*Makofi*)

Mheheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umepata msaada mkubwa sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na tunawashukuru sana sana kwa jinsi walivyochangia, wakitumia uwezo wao, nafasi waliyokuwa nayo katika Bunge hili na nafasi ya kuishauri Serikali. Nakiri kwamba, Bunge limeitumia vizuri nafasi yake na hiyo ndiyo kazi ambayo tumekabidhiwa na wananchi kuifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kwa kutumia Kanuni Na. 87(1); naomba kuisoma inasema: “Endapo Muswada ulikwishesomwa mara ya pili na haukuwa na mabadiliko lakini kuna jambo au suala jipya limetokea na linahitaji kuzingatiwa, mtoa hoja anaweza kumwomba Spika wakati wowote kabla Muswada haujapelekwa katika Kamati ya Bunge Zima kwamba Muswada huo urejeshwe tena kwenye Kamati inayohusika.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa na taadhima, naomba nitumie kifungu hiki kwa kukuomba wewe ukubali niurejeshe Muswada huu katika Kamati kwa muda na tupangiwe muda wowote katika kipindi hiki cha Bunge tuweze kuendelea na Muswada huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kwa mujibu wa kifungu hicho cha 87 ambacho kimewekwa sawa, Mheshimiwa Naibu Spika anakubali kwamba, Muswada huo urudishwe kwenye Kamati. Sasa naagiza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na wale wote ambao walikuwa na maoni kuhusiana na Muswada huu, washiriki katika kuuboresha Muswada huu na nitapewa taarifa kwamba sasa Muswada uko tayari. Kwa hiyo, Muswada tumeahirisha kwa maana hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunaendelea kujifunza wote, Mheshimiwa Dkt. Slaa katika mchango wake alitumia kifungu cha 69 cha Kanuni zetu. Kifungu hiki cha 69(1) na (2) kinasema: “Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja, maneno yanayotakiwa kusema kwamba sasa mjadala uahirishwe. Ndiyo anafunga maneno yake. Na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.” Kifungu cha 69(2) kinasema: “Kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, atakataa kuitoa iamuliwe.”

Kwa hiyo, ndivyo nilivyofanya. Nilikataa kutoa iamuliwe kwa sababu nilifikiri kwamba, baada ya kusikiliza watu wanasema, hakuna ubishi wala hakuna aliyebisha. Kwa hiyo, nilikuwa nasubiri kwamba nisilete uanzu kushindana juu ya kwamba uletwe au usiletwe. Kwa hiyo, nilitumia hiyo na zaidi haikuletwa kama hoja, alikuwa anachangia katika sehemu ya mchango wake. Kwa hiyo, sasa maamuzi yetu ni hayo kwamba, Muswada huu urudi kwenye Kamati na Kanuni hizo hizo zinataka wale watakaokuwa wameona wameguswa sana na Muswada huu na wana maoni yao kama walivyotoa hapa, washiriki kwenye Kamati hiyo; kama siyo Wajumbe wa Kamati hiyo hawana mamlaka ya kupiga kura, watachangia lakini hawatapiga kura kwenye Kanuni hiyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nadhani tumefikia pazuri.

Sasa nina matangazo yafuatayo: Nina tangazo la Mheshimiwa Dkt. Chegeni, kwa niaba ya Mwenyekiti Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, wakutane katika kikao cha pamoja leo hii tarehe 30 Januari, 2010. Mnaweza kukutana kuanzia sasa hivi katika Ukumbi wa Pius Msekwa, hapa waliweka saa saba sasa mnaweza kuanza sasa hivi.

Halafu Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge, Bwana John Joel, kuna Kamati ya Uongozi wa Bunge tarehe 1 Februari, 2010 saa 5.00 asubuhi kwenye Ukumbi wa Spika ili kutathmini mwenendo wa shughuli za Mkutano uliobaki.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo mimi sina jingine. Napenda kuwashukuru kwa kazi mliyofanya wiki yote hii. Naona Waheshimiwa wamefanya kazi ya kusoma sana na kuishauri Serikali ipasavyo na kwamba sasa niwatakie wikiendi njema. Tukutane Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 4.55 asubuhi Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,
Tarehe 1 Februari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*